HOTUBA YA MHESHIMIWA HAWA A. GHASIA (MB), WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWENYE UZINDUZI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA YANAYOFANYIKA MKOANI KATIKA MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI TAREHE 26 JUNI, 2015

Mheshimiwa Halima Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara,

Mheshimiwa Dkt. Didas Massaburi, Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT),

Mheshimiwa Balozi Masaharu Yoshida, Balozi wa Japan,

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mtwara - Mikindani;

Mheshimiwa Naibu Waziri, OWM - TAMISEMI,

Katibu Mkuu, OWM - TAMISEMI, Ndugu Jumanne Sagini,

Manaibu Katibu Wakuu mliopo,

Katibu Mkuu ALAT –Taifa,

Waheshimiwa Wabunge mliopo,

Wakuu wa Wilaya mliopo,

Viongozi na Wawakilishi kutoka Mashirika, Makampuni na Taasisi zilizofadhili maadhimisho haya,

Viongozi wa Vyama vya Siasa mliopo,

Wanahabari,

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

UTANGULIZI:

Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana leo katika uzinduzi wa maadhimisho ya Siku ya Serikali za Mitaa Tanzania yanayofanyika hapa Mtwara-Mikindani. Pili, napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha washiriki wote kwenye maadhimisho haya muhimu yenye lengo la kujipima wapi tulipotoka, wapi tulipo sasa na mwelekeo wa baadaye katika kutekeleza jukumu letu kuu na la msingi la utoaji huduma bora kwa wananchi.

Tatu, naomba nitumie nafasi hii kuwapongezeni sana kwa maandalizi mazuri ya maadhimisho haya ambayo sote tunatarajia kwamba yatafana. Mkoa wa Mtwara umepata heshima kubwa ya kuwa mwenyeji wa maadhimisho haya, kwa kuwa Halmashauri zote nchini pamoja na Wadau mbalimbali wa maendeleo wamepata fursa ya kuja Mtwara, kwa ujio wenu hapa hamtakosa jambo la kujifunza kutoka Mtwara kutokana na sifa nyingi za Mkoa huu, zikiwemo fursa za uwekezaji kwenye Sekta ya Gesi. Hali kadhalika sisi wana Mtwara hatutakosa jambo la kujifunza kutoka kwa wageni wengi waliofika hapa Mtwara.

Mwisho, japo siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru sana Serikali ya Japan kwa kusaidia mageuzi ya Serikali za Mitaa husan kwa kupitia mafunzo kwa Viongozi na Watendaji wa Serikali za Mitaa, Mikoa pamoja na Wizara, natambua pia mchango wenu katika program ya upangaji wa mipango kwa kutambua fursa na vikwazo (O & OD) Program hii imekuwa ni chachu ya upangaji wa mipango inayozingatia mahitaji halisi

ya wananchi katika Vijiji pamoja na mengine mengi, tunasema asanteni sana na tunawashukuru kwa ushirikiano wenu.

Aidha, ninapenda kuwashukuru Wabia wote wa Maendeleo wanaoshirikiana na Serikali katika kuleta magezi ya mifumo na utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, hakika tunatambua mchango wenu, asanteni sana.

Pia, kuwashukuru wote ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia ufanisi wa maadhimisho haya. Ninaamini kuwa mmekuwa na vikao vingi vilivyowezesha kuamua kupanga na kutekeleza haya tunayoyaona leo. Ni wazi kwamba, mmetumia raslimali nyingi zikiwemo fedha na nguvukazi pamoja na muda wa viongozi na wataalamu sambamba na nguvu za wananchi wa Mkoa huu kuweza kufanikisha shughuli hii na nyinginezo muhimu hadi kufikia siku ya kilele cha maadhimisho haya hapo tarehe 01 Julai, 2015. Ninapenda niwapongeze kwa kazi nzuri mliyoifanya na mnayoendelea kuifanya ili kufanikisha maadhimisho ya siku ya Serikali za Mitaa, nasema Asanteni Sana.

Ndugu Wananchi,

Uzoefu wetu kuhusiana na maadhimisho haya ya Serikali za Mitaa unaonyesha kwamba maadhimisho haya yanatuwezesha kutoa picha halisi ya wapi tumetoka na wapi tupo sasa kwa maana ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi na hatua iliyopigwa kuhusiana na maendeleo ya Watanzania kwa ujumla, hususan baada ya miaka 31 ya kurejeshwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kila mwaka maadhimisho haya huwa na Kaulimbiu ya kutuelekeza maeneo mahsusi ya kupewa kipaumbele katika mipango yetu.

Kaulimbiu ya mwaka huu imebeba mambo makuu mawili ambayo yanajenga misingi kwa maendeleo endelevu kwa Taifa letu ambayo inasema ***"Mwananchi pigia kura Katiba Pendekezwa na Chagua Viongozi bora kwa maendeleo endelevu baada ya 2015"***.

Ndugu Wananchi,

Tunafanya maadhimisho ya Siku ya Serikali za Mitaa, baada ya kukamilisha zoezi muhimu la uchaguzi wa viongozi katika ngazi za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, ikiwa ni kipengele muhimu cha uendelezaji wa Demokrasia nchini na wakati huo huo tukijiandaa kwa ajili ya kuipigia kura ya maoni Katiba Pendekezwa na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Napenda nitumie fursa hii kuziagiza Mamalaka zote za Serikali za Mitaa nchini kufanya yale yote yatakayofanikisha mazoezi hayo, ikiwemo kudumisha hali ya ulinzi na usalama ili wananchi waweze kushiriki katika hali ya amani na utulivu.

Ndugu Wananchi,

Katika maadhimisho ya siku ya Serikali za Mitaa, imeonyeshwa kuwa kutakuwepo na maonesho ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Aidha, Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali pamoja na Wadau wa maendeleo watapata fursa ya kuonesha shughuli

wanazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yao ya kuchangia ukuaji wa uchumi na utoaji huduma bora kwa jamii.

Pia, napenda kusema wazi kuwa maonesho hayo ni nyanzo muhimu sana katika kujenga mtandao wa wazalishaji na watoa huduma katika Mkoa wetu wa Mtwara, na nchi yetu kwa ujumla. Hii ni fursa nzuri kwa kuelimishana na kuwezeshana katika kuboresha huduma zetu na vilevile kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Napenda kutoa wito kwa wananchi wote kutembelea mabanda mbalimbali ya maonesho na kudai maelezo ya kutosha kutoka kwa waoneshaji. Aidha, niwaombe waoneshaji kuwepo kwenye mabanda yao muda wote na kutoa maelezo kwa kadri wananchi watakavyoyitaji.
Napenda kusisitiza kuwa maadhimisho ya Siku ya Serikali za Mitaa yana umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya wananchi wetu na vilevile katika ukuaji wa uchumi. Ni jukumu la Jumuia ya Tawala za Mitaa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali na wadau wengine kuona kuwa maadhimisho haya yanaboreshwa kwa kila namna na yanaundiwa mkakati wa upatikanaji wa

fedha. Taarifa nilizonazo zipo baadhi ya Halmashauri zinasuasua kuchangia maonesho haya tangu miaka iliyopita na hata haya ya mwaka huu. Ni vema Halmashuri zitenge fedha katika bajeti zao za kila mwaka kwa kazi hii.

Ndugu Wananchi,

Mwisho, napenda nimalizie kwa kuwashukuru tena wenyeji wa maadhimisho haya ambao ni wananchi wa mkoa wa Mtwara wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Halima Dendego, akisaidiwa na Katibu Tawala wa Mkoa Ndugu Alfred Luanda na timu yake katika Sekretariati ya Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Viongozi wengine wa Wilaya na Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote za Mkoa huu.

Baada ya kusema hayo niwashukuruni wote mliohudhuria hafla hii na ninayo furaha kutamka kwamba maadhimisho ya Siku ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2015 yamezinduliwa rasmi hapa Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.